THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI

SEHEMU A

Zoezi la 2

Kusoma kwa Sauti

Gredi ya 5-2026

NAKALA YA MWANAFUNZI

© 2026 The Kenya National Examinations Council

Zainabu anapenda sana kupika. Siku moja, aliamua kupika chakula cha jioni. Alienda sokoni akanunua vyakula mbalimbali. Alinunua mboga, ndizi na samaki. Aidha, alinunua viungo vya kupikia vikiwemo vitunguu, nyanya na iliki.

Jioni hiyo, Zainabu alipika kwa bidii na nidhamu. Alitumia viungo jinsi alivyotazama kwenye mtandao. Alitumia viwango vya joto vilivyofaa. Alitaka kuhifadhi virutubishi vyote muhimu katika vyakula alivyovipika.

Kila mmoja katika familia yake alivutiwa na harufu nzuri kutoka jikoni. Wakati wa kuandaa chakula ulipofika, Zainabu alikuwa tayari. Aliwaita ndugu zake ili waje kumsaidia kupanga meza.// Familia nzima iliketi mezani na kula kwa furaha. Wote walikula wakashiba. Walipendezwa na upishi wake ambao waliuthamini sana. Wote walimpongeza Zainabu. Zainabu aliwashukuru kwa kumpongeza.

© 2026 The Kenya National Examinations Council